

Kumbadilisha mtu aliyeathirika na dawa za kulevya

By SW - Melkisedeck Shine · April 17, 2022

Ujana na Makuzi | Mapenzi na Ngono Salama

Endapo rafiki au jamaa anaomba msaada wa kuacha kutumia dawa za kulevya unaweza kumsaidia kwa kumpatia nasaha. Jitahidi kumpatia taarifa zote muhimu kuhusu dawa za kulevya. Muhimu zaidi mweleze athari za matumizi ya dawa hizo. Hata wazazi unaweza kuwapatia ushauri endapo watatambua umuhimu wako wa kujali. Wakati mwingine waathirika wa dawa za kulevya hawako tayari kusikiliza ushauri na msaada wako. Inaweza kutokea muathirika akawa na hasira na hata kuvunja urafiki wenu na hata kufa. Usijilaumu!!! Kwa sababu ulijitahidi kumsaidia kadri ya uwezo wako. Wakati mwingine ni vyema kuvunja urafiki kwa usalama wako na kwa faida ya rafiki yako. Rafiki huyo anaweza kugundua kuwa utumiaji wa dawa za kulevya unamletea mwisho mbaya na hatimaye kuchukua uamuzi wa kueleza matatizo yake. Kama itatokea rafiki au ndugu yako ambaye ni teja ameathirika sana kiafya usijaribu kumsaidia peke yako. Inaweza kuwa muhimu kumtafutia msaada wa kitaalamu kutoka kwa mtaalamu.

Printable AckySHINE Article · <https://ackyshine.com/post.php?post=25872>